



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA



Taarifa namba: 044

01/10/2022

TAARIFA KWA UMMA

TAARIFA YA MAKUSANYO YA MAPATO KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA YA MWAKA WA FEDHA 2022/23

Halmashauri ya Mji Tunduma inapenda kuutaarifu umma kuwa katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka yaani, mwezi Julai hadi Septemba ya mwaka wa fedha 2022/23, imekusanya Shilingi Bilioni 3,702,234,705.65/= sawa na ufanisi wa 176.31% ya lengo la kukusanya Shilingi Bilioni 2,099,900,000/=

Kwa mwezi Julai - Septemba 2022, Halmashauri imekusanya Zaidi ya lengo ukilinganisha na makisio ya mwezi husika.

1. Mwezi Julai Halmashauri ilikusanya kwa ufanisi wa 152.0 %,
2. Mwezi Agosti Halmashauri ilikusanya kwa ufanisi wa 176.6%
3. Mwezi Septemba Halmashauri ilikusanya kwa ufanisi wa 200.4%

Jedwali Na. 1: Makusanyo ya Mapato katika Robo ya Kwanza, 2022/23

MWEZI	MAKISIO	MAKUSANYO	ASILIMIA	UFANISI	ONGEZEKO LA UFANISI
JULAI	699,966,666.67	1,063,838,824.04	152.0%	363,872,157.37	52%
AGOSTI	699,966,666.67	1,235,979,884.73	176.6%	536,013,218.06	76%
SEPTEMBER	699,966,666.67	1,402,415,996.88	200.4%	702,449,330.21	100.4%
JUMLA	2,099,900,000	3,702,234,705.65	176.31%	1,602,334,705.64	76.31%

Aidha kwa lengo la mwaka wa Fedha 2022/2023 mpaka sasa kwa Robo ya kwanza kuanzia Julai – Septemba Halmashauri ya Mji Tunduma imefanikiwa kukusanya jumla ya 44.1% kwa ufanisi wa Ongezeko la 19.1% kutoka kwenye lengo la mwaka la kukusanya 8,399,600,000/=

Jedwali Na. 2: Makusanyo ya Mapato katika Robo ya Kwanza Dhili ya
Makusanyo ya Mwaka, 2022/23

MWAKA	MAKISIO	MAKUSANYO KWA ROBO	ASILIMIA	UFANISI	ONGEZEKO LA UFANISI
2022/2023	8,399,600,000	3,702,234,705.65	44.1%	1,602,334,705.64	19.1%

Halmashauri ya Mji Tunduma inawashukuru **Taasisi za Umma, Taasisi Binafsi, Makampuni, wafanya biashara wakubwa, wafanya biashara wadogo na Wananchi kwa ujumla** kwa ushirikiano mkubwa wa kulipa Tozo halali za serikali zilizowekwa kwa mujibu wa sheria nchi.

Pia Halmashauri inawakumbusha wale wote ambao bado hawajalipa **Kodi ya pango, Leseni za Biashara, Ushuru wa Huduma, Ushuru wa malazi, Tozo ya usafi wa mazingira, ada za maegesho, Stika za vyombo vya usafiri, Ushuru wa Mazao** na ada mbalimbali kulipa kwa wakati ili kuirahishia Halmashauri kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wananchi wa Tunduma.



WILLIAM MAGANGA

**KAIMU MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
HALMASHAURI YA MJI-TUNDUMA.**